





Hapo zamani,  
kulikuwa na mvulana  
kwa jina Petro.  
Alikuwa mwanafunzi  
mwerevu aliyeibuka  
wa kwanza  
darasani. Wazazi wake  
walijivunia kazi  
yake nzuri. Lakini,  
Petro alitamani  
kuwa na kaka, dada au  
hata kipenzi  
cha kucheza naye.





Siku moja, Petro  
alimwuliza mama,  
"Ninaweza kwenda nje  
kucheza?  
Nimekuwa nikisoma  
wakati huu wote.  
Ningependa sasa  
niende nicheze na  
marafiki zangu."  
Mamake alimjibu, "Ni  
sawa! Nenda, lakini  
usichelewe!"



Alipokuwa akienda  
uwanjani, Petro  
aliona jambo  
lisilokuwa la kawaida.  
Alimwona mbwa  
mdogo mwenye  
madoadoa. Mbwa  
huyo alikuwa  
amekwama shimoni  
na alikuwa  
ameogopa. "Usiwe na  
wasiwasi,  
sitakuumiza.  
Nitakusaidia," Petro  
alimwambia.



Petro alimtoa mbwa  
yule shmoni.  
Mbwa alibweka kwa  
furaha, akacheza  
cheza na kumlamba  
Petro. "Utakuwa  
mbwa wangu," Petro  
alisema kwa  
furaha.



Mbwa alikimbia akaenda mbali na Petro. Marafiki za Petro walipomwona mbwa akiwakaribia, walisema, "Mbwa huyu anaweza kutuumu." Walimpiga kwa mawe. Petro alipowaona, alikimbia akiwapigia kelele waache kufanya hivyo.




Marafiki wale  
hawakumsikia Petro.  
Mbwa alikimbia  
haraka alivyoweza ili  
kuyaokoa maisha  
yake. Alijificha ili  
wavulana wale  
waliokuwa  
wakimfukuza  
wasimwone.  
Hawakumpata.



Marafiki wa Petro walirudi uwanjani na kumkuta Petro akiwa analia. "Kuna nini?" mmoja wao aliuliza.  
"Mlimfukuza mbwa wangu!" Petro alieleza. Walishangaa na kusema,  
"Hatukujua kwamba yule aliquwa mbwa wako.  
Tunakuomba radhi.  
Twende tumtafute."



"Hakuna maana ya kufanya hivyo.  
Hatutawahi kumpata,"  
Petro alisema  
kwa huzuni. "Ndiyo,  
tutampta. Amka twende, tutampata  
mbwa wako.  
Tusipoteze matumaini," marafiki  
zake walimfariji.



Petro na marafiki zake  
walimtafuta  
mbwa kwa muda  
mrefu hadi  
wakachoka. Hatimaye,  
Petro alisema,  
"Kuna sehemu moja  
ambapo anaweza  
kuwa amejificha.  
Tusipompata huko,  
sitamtafuta tena.  
Twendeni mtoni."



Mbwa alipowaona  
wavulana wakija,  
aliogopa tena. Aljaribu  
kuvuka mto  
lakini vilevile  
aliyaogopa maji.  
Alikuwa  
karibu kuruka majini,  
wakati Petro  
alisema, "Acha,  
usiruke!"



Mbwa alipogeuka na kumwona Petro, alimkimbilia. Petro alimkumbatia mbwa wake naye mbwa akamlamba usoni. "Rafiki yangu! Nilidhani kwamba umepotea kabisa!" Petro alilia.



Walipokuwa uwanjani,  
Petro  
aliwashauri marafiki  
zake. "Kabla ya  
kuamua kutenda  
jambo, tafadhali  
fikirieni kinachowezza  
kutokea.  
Mnaweza kuwaumiza  
wenzenu."  
Marafiki zake waliwaza  
juu ya maneno  
yake kisha wakasema,  
"Tusamehe.  
Mbwa huyu atakuwa  
rafiki yetu pia."